

Biashara Ndogo ya Afrika ya Mashariki

Basma F.

Insha hii inahusu biashara ndogo za Afrika ya Mashariki. Mimi ninapenda biashara ndogo kwa sababu ninasadiki biashara ndogo zinasaidia watu, mmoja mmoja. Biashara ndogo hufaidi wanaume na wanawake, jamaa zao na jamii zote kwa jumla. Kama watu wamemiliki kazi wenyewe, huwa nzuri sana. Kwa mimi, kama nimefanya vitu vyangu mwenyewe ninajua ni tofauti na kufanyiwa na mtu mwingine. Kama mtu atasafiri Afrika ya Mashariki, labda ataona biashara kama:




Biashara za Ukulima

Wakulima, kama Jacinta, wanakuza mimea na miti. Kilimo ni biashara muhimu kwa sababu hakuna hata mmoja anayejua hali ya kesho. Labda, kutakuwa na jua au mvua. Kuna hatari wakati wa kutegemea hali ya anga. Wakulima, wanachuma pesa wakati wa kuuza matunda ya mimea na miti – kama machungwa, maembe, mapapai, nazi, mananasi na mengine – sokoni, baada ya mavuno.

Biashara za Uvuvi

Wavuvi ni wakulima wa maji! Wavuvi wanavua samaki. Wavuvi wanafanana na wakulima kwa sababu wanachuma pesa wakati wa kuuza “matunda” ya mto, ziwa, na bahari. Susan ni mvuvi mashuhuri, na pia anapika samaki mafutani – basi, Susan ana hoteli ndogo ya kuuza samaki na viazi vitamu!



Biashara za Ushonaji

Ushonaji ni biashara kubwa Afrika Mashariki. Kwa mfano, George ni mshonaji, na anachuma pesa sana kwa sababu anashona mavazi mapya, lakini anauza mavazi ya “mtumba.” Licha ya hayo, George anatengeneza mavazi yaliyoraruka. Wakati wa kushona mavazi kwa wanafunzi, washonaji wanafurahi kwa sababu wanafunzi wanahitaji sare mpya mwaka baada ya mwaka.

Biashara za Uchuuzi

Magdalene ni mchuuzi wa vyombo vya nyumbani. Magdalene ni mchuuzi maarufu. Nna anafikiri: Watu wanahitaji nini kwa nyumba?? Anapata vitu vyote wanunuzi walitaka. Kwa mfano, wanunuzi wanataka kupata bakuli au vijiko, Magdalene ana vitu hivi.




Biashara za Mifugo

Wafugaji wanahudumia wanyama. Sammy ni mfugaji, na ana mbuzi wengi. Sammy anauza mbuzi sokoni kwa wafugaji wengine au labda kwa wachinjaji. Sammy ana furaha hasa wakati mbuzi wanaponenepa kwa sababu mbuzi wakubwa wanampa Sammy pesa nyingi! Sammy anafanana na mkulima kwa sababu anapenda wakati wa mbuzi kusitawi, kama mkulima anapenda wakati wa mimea inamea.

Biashara za Utajiri

Matajiri ni makabaila kwa biashara. Matajiri wanaongoza kwa chaji ya vitu. Francis ni tajiri, kwa makaa. Watu wanataka makaa kwa kuwasha moto, kupika chakula na kuchemsha maji na kunawa. Francis anaitwa tajiri kijijini kwake, lakini Francis ni tajiri mdogo; anauza makaa kwa wengine, lakini tajiri mkubwa labda anauza makaa kwa maduka madogo.



Biashara za Upishi

Rose ni mpishi. Anapenda kupika chakula na chakula chake ni kitamu! Anapika mandazi, chapati, chipsi, kuku, mbuzi, chai, wali, na ugali. Watu wanapenda kula katika hoteli ya Rose kwa chamshakinywa, chakula cha mchana, na chajio, na kama wanataka kula makumbwe.